

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**KIKAO CHA NANE**

**06 FEBRUARI, 2025**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

### MKUTANO WA KUMI NA NANE

**KIKAO CHA NANE – TAREHE 06 FEBRUARI, 2025**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

### **III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:**

### **IV. MASWALI YA KAWAIDA:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

#### **128. MHESHIMIWA KHADIJA SHAABAN TAYA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Wakuu wa Wilaya wametokeleza kwa kiasi gani agizo la Waziri Mkuu la kutenga ofisi za Watu wenye Ulemavu katika ofisi zao.

#### **129. MHESHIMIWA SUBIRA KHAMIS MGALU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Maafisa Masuuli na Wahazini wa Serikali za Mitaa kutokana na ongezeko la Hoja za ukaguzi za Ripoti za CAG.

**130. MHESHIMIWA SAMWELI XADAY HHAYUMA (HANANG’):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mkakati wa Serikali kuboresha Zahanati za zamani zilizopo Makao Makuu ya Kata za Hanang’.

**131. MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga Shule mpya ya Sekondari katika Kata ya Mabogini Moshi Vijijini.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**132. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Tanzania itaridhia Mkataba wa Kujikinga na Bidhaa za Nyuklia (*Convention on the Physical Protection of Nuclear Material*) wa Julai, 2005.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **133. MHESHIMIWA CECILIA DANIEL PARESSO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuondoa tatizo la upungufu wa maji katika Mji Mdogo wa Karatu.

## **WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

### **134. MHESHIMIWA PROF. PATRICK ALOIS NDAKIDEMI (MOSHI VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani kuwasaidia Wananchi wa Jimbo la Moshi Vijijini kuzalisha asali kwani kuna idadi kubwa ya miti inayoweza kutundikwa mizinga.

### **135. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itapeleka Askari wa kutosha wa Jeshi la Uhifadhi Tunduru Kaskazini ili kumaliza athari zinazosababishwa na Wanyama Pori.



## **WIZARA YA AFYA:**

### **136. MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT MATHIAS GWAJIMA (KAWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itaanza Matibabu ya Wagonjwa Wenye Seli Mundu kwa kutumia *Crispr Gene Editing Technology*.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **137. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINA CHRISTOPHER MNZAVA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Old Shinyanga hadi Solwa utaanza.

## **V. HOJA ZA KAMATI:**

### **MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA  
BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA  
USALAMA:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**DODOMA  
06 FEBRUARI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD  
KATIBU WA BUNGE**

